


Mbuguma na Nasiru



Sharifa Y. Shemputa



Mbuguma na Nasiru

Sharifa Y. Shemputa



Toleo la kwanza la kitabu hiki lilichapishwa kwa Kiswahili na Kiingereza na Readership for Learning and Development - **Soma** kwenye mfululizo wake mpya wa *Kalamu Ndodo*.

Kimeandikwa na Sharifa Shemputa kwenye utafiti na uandishi uliowezeshwa na mradi wa **Soma** wa Watoto na Vitabu uliofadhliliwa na Neil Butcher & Associates.

Michoro na Khalid Yusuf, Usanifu umefanywa na Eva Gervas Kimehaririwa na Demere Kitunga, Godfrey Mishomari na Latifa Miraji.



Hakimiliki ya kitabu hiki inamilikiwa kwa pamoja na wabunifu wake na Kiota cha Simulizi cha Watoto na Vitabu cha **Soma**, ambao wameridhia kuweka baadhi ya haki zao kwenye leseni ya Creative Commons Attribution 4.0 license. Hii ina maana kwamba, yejote ana uhuru wa kupakua, kufasiri, kupiga chapa na kusambaza kitabu hiki kwa masharti kwamba anawatambua wenye hakimiliki.

ISBN 978-9976-5637-8-8

Tahariri

Mbuguma na Nasiru ni hadithi ya nne ya ‘Kalamu Ndodo’, mfululizo mpya wa **Soma** wa vitabu vya watoto vilizoandikwa na watoto. Vitabu vinne vya kwanza katika mfululizo huu ni zao la mradi wa utafiti na uandishi wa Kiota cha Simulizi cha Watoto na Vitabu, uliofadhliliwa na Neil Butcher & Associates. Kiota hiki ni sehemu ya Mkahawa wa Vitabu wa **Soma**; kinachopokea watoto wa miaka 6 hadi 13.

Mradi huu unachangia juhud za Shirika la William and Flora Hewlett Foundation za kuimarisha ngazi ya awali ya usomaji; kwa kuwezesha na kuhifadhi taarifa za mafanikio ya miradi ya majaribio na ubunifu katika kuandaa na kusambaza matini bora ya usomaji kwa mfumo wa hakimiliki shirikishi barani Afrika.

Mkahawa wa Vitabu **Soma** ni taswira ya **Soma**. Ni nafasi jumuishi ya usomaji na fasihi kwa burudani, utamaduni na maarifa, iliyoanzishwa mwaka 2008 Jijini Dar es salaam. **Soma** ni shirika lisilo la kiserikali kwa jina rasmi E&D Readership and Development Agency hadi mwaka 2019; na baadaye Readership for Learning and Development. Dira ya **Soma** ni kuona ‘utamaduni wa Vijana na Watoto wa Tanzania ikiwa ni umahiri katika usomaji, simulizi na utafutaji vikiwa’.

Mradi huu ulizingatia uwezo na ubunifu wa watoto. Waliwezeshwa na waandishi wa vitabu vya watoto, walimu, wahariri, wachoraji na wasanifu, kulitafiti, kuliandika, kulipitia, kulihariri, kudurusu na kupendekeza michoro ya hadithi zao. Hadithi hizi ni za kisasa waizoziibua kutoka kwenye ngano za mapokeo, uzoefu wao kama watoto na njozi na matamano yao mbali na muktadha wa sasa. Tunawiwa shukurani za dhati kwa jumuia hii ya wanafasihi kwa kutufunza. Kwa Lisbeth Levey (Liz) kwa kutuamini. Neil Butcher & Associates kwa rasilimali za kufanikisha mradi huu na kwa kutuunganisha na Mtando wa


Elimu ya Awali (Early Literacy Resource Network). Liz, Kirsty von Gogh na Ken Harley kwa kutuhimiza na kututia moyo bila kuchoka.

Tunawashukuru watoto wote walioshiriki, wazazi, walimu na wawezeshaji kutoka Watoto na Vitabu na Kituo cha Elimu HK na Sanje-Mwenge kwa kujitoa na uvumilivu wao; wawezeshaji na wataalamu mbalimbali: Godfrey E. Mishomari, mwezeshaji kiongozi wa Utafiti na Uandishi; Gonsalves Mpili, Maria Mrindoko, Latifa Miraji, (wawezeshaji wenza); Patrick Gongwe na Alphonse Mapunda (Wakuu wa Vituo); Nadir Tharani (mwandishi, mchoraji na msanifu wa vitabu vya watoto) walioshirikiana nasi katika hatua ya uhariri; na Mohamed Ismail, picha za mnato na video; Paulina George na Invioleta Mwakiwone kwa mchango wao wa mawazo, uendeshaji, kuchukua picha za matukio na kuzisambaza; Mugisha Bassasingohe kwa msaada wa Tehama; na Ubongo Kids kwa kutupa uzoefu wao. Hatimaye, vionjo vya mradi huu vinapatikana kwenye tovuti yetu www.somabookcafe.com.

Mbuguma na Nasiru imeshika nafasi ya nne kati ya hadithi 40 zilizoandikwa na watoto. Michoro ya Khalid Yusuf imezingatia maelekezo ya mwandishi, na uhariri ulikuwa kidogo na shirikishi ili kuhuisa sauti mtoto. Idhini ya mzazi na ridhaa ya mtoto vilizingatiwa.

Mapato kutokana na kitabu hiki kama yatakuwepo yatachangia kuendeleza mradi huu. Tuliifanya kazi hii kwa mapenzi. Tunaamini itapendwa pia na wasomaji na waelimishaji; vinginevyo itabakia kuwa hekaya nzuri ya ndotoni.

**Demere Kitunga,
Februari 2020, Dar es Salaam**



Hapo zamani za kale palikuwapo na mtoto wa Bi Mkubwa na mtoto wa Bi Mdogo. Wote walikuwa wa kiume wa miaka saba.

Mtoto wa Bi Mkubwa aliitwa Mbuguma na wa Bi Mdogo aliitwa Nasiru.


Watoto hao na mama zao waliishi katika kijiji cha Ngaramo.

Siku moja wazazi wao waliugua ugonjwa wa ghafla.
Ngozi zao zilikuwa na vipele vikubwa kama majipu. Wote wawili
waliwaita watoto wao na kuwatuma kwenda msituni kutafuta dawa.



Asubuhi ya siku iliyofuata Mbuguma na Nasiru walielekea msituni.
Walifika njia panda. Walikubaliana kugawana njia na kukutana
hapo siku inayofuata.





Mbuguma alikutana na mwindaji.
“We mtoto unatafuta nini msituni huku?”


“Natafuta mti dawa ya ngozi
itakayomtibu mama yangu.
Tafadhal naomba unioneshe dawa hiyo.”

Alimwelekeza mti wa
dawa na kumpa masharti.

“Ukishapata dawa
usigeuke nyuma wala
kurudi nyuma
hata kama utasikia
sauti yoyote.”



Alipofika alichuma dawa na kurudi. Njiani alisikia sauti.
“Ukigeuka nyuma nitakupa dhahabu, maisha mazuri na
mzazi wako atapona.” Hakugeuka nyuma.
Ile sauti ilijirudia tena. Hakugeuka nyuma.



Ile sauti ilijirudia tena na tena.
Mbugama akageuka nyuma.
Aliona mwanga mkali.
Sauti ikamwambia,
“Ufuate huu mwanga”

Ule mwanga ulimpeleka
katikati ya msitu.
Hakujua alikotokea wala njia
ya kurudi nyumbani kwao.








Usiku ulipofika aliona mwanga mkali katikati ya msitu.
Chini yake alimwona mdogo wake akichuma dawa.
Alimuona pia mama yake akiwa kitandani lakini akiwa na furaha.


Alijaribu kuusogelea ule mti lakini alishindwa kwani mwanga ulikuwa
mkali sana. Upepo mkali ulivuma ukamchukua na kumtupa mbali.
Akapitiwa na usingizi mzito.




Nasiru njiani alikutana na Mkulima.
“Unatafuta nini huku mtoto
mdogo wewe kwenye msitu
huu wa maajabu?”



“Natafuta dawa ya kuponya
ugonjwa wa mama yangu.”
Mkulima alimpeleka kwenye ule mti
na akapata dawa.
“Ukishachukua hiyo dawa ukisikia
sauti yoyote ile usigeuke nyuma.”





Alipokuwa akirudi alisikia
sauti ikisema
“Ukigeuka nyuma nitakupa
dhahabu, maisha mazuri
na mzazi wako atapona.”
Nasiru hakujali.

Aliendelea kuisikia sauti ile ikijirudia masikioni mwake. Alitamani kugeuka lakini alikumbuka hali ya mama yake. Alijipa moyo na kuendelea hadi alipofika sehemu walipoachana na kaka yake. Alishangaa hakumkuta kaka yake.








Aliamua kupeleka dawa nyumbani.
Alipofika nyumbani alitengeneza na
kuwapatia dawa wazazi wake.
Kisha alirudi msituni kumtafuta kaka yake.



Alipofika njia ya panda alipita njia ile aliyopita kaka yake.
Mbele kidogo alikutana na mwindaji.




“Unatafuta nini wewe mtoto mdogo
katika msitu huu mkubwa?”
“Samahani namtafuta kaka yangu
alikuja msituni kutafuta dawa.
Je, ulimwona kaka yangu



Mwindaji alimhadithia ilivyokuwa.
Mwishowe alisema.
“Ukimpata kaka yako mwambie
awe na msimamo na aache tamaa.
Matatizo yaliyomkuta ni kwa
sababu hakuwa na msimamo.”

Mwindaji alimpeleka Nasiru
alipokuwa kaka yake.
Walirudi nyumbani pamoja.
Njiani Mbugama alimsimulia
mdogo wake yaliyomkuta naye
alimsimulia aliyokutana nayo.



Wazazi walifurahi kuwaona
watoto wao wamerudi salama.





Mbuguma na Nasiru ni Ndugu, baba mmoja mama mbalimbali. Ni watoto wadogo lakini lazima wafunge safari ya hatari. Kwa nini? Mama zao ni wagojwa kitandani. Wametumwa kwenda mwituni kuwatafutia dawa. Wanapofika njia panda na kuamua kila mmoja ashike njia yake, kila mmoja anaponywa au kuponzwa na tabia yake.

Sharifa Y. Shemputa, mwandishi wa hadithi hii ni msichana wa miaka 13. Anasoma darasa la Saba. Anapenda kusoma, kuandika hadithi na kuchora. *Mbuguma na Nasiru* ni kitabu chake cha kwanza kuchapishwa.

Vitabu vingine katika mfululizo huu:

- *The Lonely Frog*
- *Chura Mpweke*
- *The Poor Lady*